# Juhudi za Fasihi katika Kukabiliana na Janga la *UKIMWI*: Kifani cha Riwaya ya *Ua la Faraja*

*Arinaitwe Annensia*[1] *na Mosol Kandagor*[2]
[1]*Chuo Kikuu cha Makerere*
[2]*Chuo Kikuu cha Moi*

**Ikisiri**

**Janga la UKIMWI (Ukosefu wa Kinga Mwilini) limekuwa katika bara la Afrika kwa muda sasa. Licha ya kuzuka kwa majanga mengine ya kiafya kama saratani, korona, kisukari miongoni mwa mengine, UKIMWI bado unatishia kudumaza mustakabali wa bara Afrika. Hali hii inatokana na maambukizi yake kusambaa na kuongezeka kila uchao. Mikakati kadhaa imewekwa na Shirika la Afya Duniani (World Health Organization-WHO) ikiwemo kuwaelimisha watu kuepuka maambukizi ya ugonjwa huu kama hatua ya kukabiliana nao. Fasihi ni mojawapo katika nyenzo hizi zinazotumiwa kufundisha na kuielekeza jamii. Ni kwa misingi hii ambapo makala haya yamezuumu kudadisi na kutathimi mchango wa fasihi ya Kiswahili katika mapambano dhidi ya UKIMWI. Makala haya yanahakiki riwaya ya *Ua la Faraja* (2004). Uteuzi wa riwaya hii ulifanywa kimakusudi kutokana na upekee wake wa kuliangazia janga hili kwa mapana. Makala haya hivyo basi yanachunguza namna mwandishi anavyosawiri ugonjwa huu tangu ulipochipuka duniani, namna unavyoambukizwa, athari zake kwa umma na jinsi ya kuepuka maambukizi yake. Mwisho, makala yanadhihirisha kuwa licha ya hatari inayoletwa na ugonjwa huu, yapo matumaini makubwa katika udhibiti wake barani Afrika.**

**Maneno Muhimu**: *UKIMWI, fasihi, afya, janga*

**Utangulizi**

Kwa mujibu wa Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO, 2019) takwimu zinadhihirisha kuwa maambukizi ya UKIMWI yanaendelea kuongezeka. Yamkini takribani watu milioni 37.9 wameambukizwa ugonjwa huo. Takwimu hizo vilevile zinaonyesha kuwa jumla ya watoto milioni 2.6 walio na umri wa chini ya miaka 15 wameambukizwa ugonjwa huu. Aidha, ripoti hii inafichua kuwa kila siku duniani watu takribani 5,600 wanaambukizwa UKIMWI huku watu 230 wakiambukizwa ugonjwa huo baada ya kila saa. Aidha, watu milioni 1.7 waliambukizwa ugonjwa huu mwaka wa 2019. Kufikia sasa idadi ya watu walioambukizwa na wanaoishi na ugonjwa huu imefika milioni 78 tangu kuchipuka kwake huku watu walioaga dunia kutokana na UKIMWI npaka sasa wakiwa milioni 39. Bara la Afrika ndilo linaloongoza kwa maambukizi ya ugonjwa huu kwa sababu asilimia 71 ya watu walioambukizwa UKIMWI ulimwenguni kufikia sasa wanatoka katika bara hili.

Kadhalika ripoti ya WHO (2019) inaonyesha haja ya bara la Afrika kulivalia njuga suala hili la UKIMWI kwa kuwa ni janga kubwa barani licha ya juhudi ambazo zimefanywa mara kwa mara kuukabili ugonjwa huu. Takwimu katika ripoti hii vilevile zinadhihirisha kuwa iwapo wadau, wahusika na wananchi wa bara la Afrika hawatakuwa makini kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huu, mustakabali wa bara hili kiuchumi, kijamii na kisiasa unaweza kudumazwa. Tahadhari kama hii inatosha kumhitaji kila mwanajamii kushiriki katika hatua na juhudi za kuukabili ugonjwa huu ili kulihakikishia bara usalama. Miongoni mwa wanajamii wanaoshiriki juhudi hizi ni waandishi wa kazi za fasihi wanaoandika kuuhusu ugonjwa huu kama mchango wao katika mapambano dhidi yake. Anavyodai Ngugi (2012:116) kuhusu dhima ya fasihi:

> *...Ni kupitia kwa fasihi ambapo msomaji wa kazi fulani hujipata kuwa amemulikwa kupitia binadamu mwingine, na akautazama ulimwengu kupitia macho ya kundi la jamii nyingine."*

Anachoeleza Ngugi hapa ni kuwa fasihi ni chombo kinachowazindua au kuwapofua watu katika jamii kupitia kwa maisha ya wahusika bunilizi na migogoro inayoibuka katika kazi hizo. Kwa

kuyaona maisha ya mhusika fulani wa kazi bunilizi ya kifasihi, mwanajamii anaweza kujirekebisha au akapata mwelekeo wa kumwongoza katika maadili maishani.

Kimsingi fasihi ni sanaa inayotumia lugha (Simiyu, 2020; Njogu, K na Chimera, R. (1999). Kwamba fasihi hutumia lugha katika kuhadili na kufafanua mambo mbalimbali yanaathiri jamii kwa namna moja au nyingine. Kama inavyobainika lugha inaibuka kuwa kifaa muhimu sana katika kukuza mawasiliano. Kandagor (2012) anaeleza kuwa lugha hutekeleza majukumu mbalimbali kutegemea launi na muktadha husika. Kuhusu nafasi ya lugha katika vita dhidi ya UKIMWI, Kandagor (2013a, 2013b) anaeleza kuwa lugha ina nafasi muhimu sana katika kukabiliana na janga la UKIMWI. Katika mkabala huo basi ni muhimu kutaja kuwa fasihi, ambayo hutumia lugha katika kuwasilisha dhana mbalimbali hutekeleza kazi muhimu sana ya kuelimisha jamii kuhusu masuala anuwai. Katika riwaya ya *Ua la Faraja*, mwandishi ametumia lugha maalum katika kuwasilisha juhudi ambazo zinaweza kuchukuliwa katika vita dhidi ya UKIMWI.

Makala haya basi yanachunguza suala la maambukizi ya UKIMWI kama linavyozungumziwa na Mkufya (2004) katika riwaya ya *Ua la Faraja* na kuonyesha namna ugonjwa huu unavyosambaa kwa kasi mno katika jamii. Uchunguzi huu unatoa tafsili kuhusu dhana UKIMWI, madai kuhusu chimbuko la UKIMWI na athari za UKIMWI katika uchumi na maendeleo ya jamii. Mwisho, makala haya yanatoa mwanga kuhusu mtazamo mpya wa bara la Afrika kuhusu ugonjwa huu.

**Muhtasari wa *Ua la Faraja***

Ua la Faraja ni riwaya ambayo imeandikwa na Mkufya (2004). Mwandishi anazungumzia maisha ya familia ya Ngoma na jirani yake Omolo. Ngoma ni mhusika aliyekengeuka na mpenda anasa. Kutokana na anasa hizo alizoshiriki, aliambukizwa virusi vya UKIMWI na mmoja wa mahawara ambaye alishiriki ngono naye. Baada ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI aliwambukiza mkewe, Tabu. Ugonjwa huu unatishia kuivuruga familia yake kiasi kwamba Ngoma anakosana na mkewe pamoja na watoto wake.

Baada ya kuambukizwa UKIMWI, Tabu, mkewe Ngoma, anatamauka. Hata hivyo, Daktari Hans, Grace (dada yake Tabu) na Omolo (jirani yake Tabu) wanamshauri na kumtia moyo kuikubali hali yake mpya ya kiafya baada ya kuambukizwa ili aweze kuishi muda mrefu na UKIMWI. Tabu anabadilisha mtazamo kuhusu UKIMWI na hatimaye anaanza kupokea matibabu, hivyo basi kuimarisha hali yake ya kiafya.

Kwa upande mwingine, Ngoma anabadilisha mkondo wake wa maisha na kuwa muumini sugu wa dini ya Kiislamu. Licha ya kuwa mfuasi mkuu wa dini ya Kiislamu, Ngoma anasalia kuwa mbishi na mgomvi. Anafarakana na watoto wake na kumgombeza mkewe kwa kushiriki dini ya Kikristo. Hatimaye anajitenga na familia yake jambo linalomfanya kukosa msaidizi hususan anapolemewa na ugonjwa. Kwa bahati, jirani yao Omolo anajitokeza na kumsaidia. Omolo vilevile anafanikiwa kuiunganisha familia ya Ngoma kwa kumpatanisha na mkewe pamoja na watoto wake.

**Dhana ya UKIMWI**

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WH.O, 2019) na Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja (2014), UKIMWI unaelezwa kuwa neno linalomaanisha upungufu wa kinga mwilini. Ugonjwa huu husababishwa na virusi vya "HIV" ambavyo hushambulia kinga ya aliyeambukizwa kiasi kwamba mwili wake hauwezi tena kujipa ulinzi dhidi ya maambukizi ya maradhi mengine nyemelezi. Kwa hivyo, watu wanaoambukizwa ugonjwa huu huwa na kinga legevu mwilini na aghalabu huathirika kwa wepesi wanapovamiwa na maradhi mengine nyemelezi.

**Madai kuhusu Usuli wa UKIMWI na Kasi ya Maambukizi Yake katika *Ua la Faraja***

Usuli wa UKIMWI unadokezwa katika riwaya ya *Ua la Faraja*. Mwandishi anamtumia mhusika anayeitwa Dkt. Hans Jumbe kueleza madai kuhusu usuli wa UKIMWI halikadhalika kutathmini kasi ya maambukizi ya ugonjwa huu. Kwa mujibu wa Dkt. Hans, usuli wa UKIMWI ni kule Marekani. Dkt. Hans anaeleza kwamba UKIMWI ni ugonjwa ulioanzishwa kimakusudi na wataalamu wa

sayansi. Baada ya kuvumbuliwa kwa ugonjwa huu, ulisambaa katika mabara ya Marekani na Ulaya. Hatimaye ongezeko la kutisha likawa Afrika ambako maambukizi yalishuhudiwa hata zaidi. Katika *Ua la Faraja*, tunasoma kuwa:

> …kama moto ulioshika kwenye msitu unapogundua chaka la majani makavu unavyopamba, ndivyo UKIMWI ulivyoivamia Afrika… (uk. 38)

Dkt. Hans anapuuza madai ya kimagharibi kuwa UKIMWI ulianzia Afrika. Anasema hivi;

> ….. ile dhana ya kwamba UKIMWI ulianza Afrika ilikuwa ni ya kipuuzi kwani ingekuwa hivyo toka mwanzo, basi kasi kubwa ya kuenea kwa ugonjwa huo ingejionyesha mara moja huku Afrika… (uk. 38-39)

Aidha, katika madai ya Dkt. Hans, kasi ya maambukizi na kuenea kwa UKIMWI barani Afrika ilikuwa na uhusiano mkubwa na matatizo ya kiutamaduni. Anadai kuwa UKIMWI uliwakuta Waafrika wengi, hasa vijana katika njia panda ya kuitamaduni. Mwafrika hujiwajibisha kutunza utamaduni wake. Baadhi ya tamaduni hizi wanazotunza huwaweka katika hatari ya maambukizi magonjwa kama ya kuambukizana yanapovamia.

Hata hivyo, suala hili la mchango wa utamaduni linaweza kudenguliwa kwa kiwango fulani inavyojitokeza katika riwaya ya *Ua la Faraja.* Mwandishi anadai kuwa mabadiliko ya kiutamaduni yameibuka kutokana na hamasisho kutoka kwa wanasiasa, vyombo vya habari pamoja na taasisi nyingine, hivi kwamba mwafrika alifumbata na kuiga mitindo ya maisha ya kimagharibi. Hapa mwandishi anaelekeza kuwa huenda huo uigaji wa mienendo na desturi za kigeni ndio uliochangia katika maambukizi hata zaidi ya UKIMWI.

Kando na uigaji huu wa tamaduni za kigeni na kupuuzwa kwa tamaduni asilia, kasi ya maambukizi ya UKIMWI ilisababishwa na mambo mengine. Mfano ni taswira ya hali katika jiji la Dar es Salaam anavyoisawiri mwandishi ambako yamkini kasi ya maambukizi ilikuwa juu sana. Anasema;

> …kasi ya kuenea kwa ugonjwa ule katika jiji la Dar es Salaam ilikuwa kubwa kuliko miji mingine. Wananadharia wengine walitoa sababu za kiuchumi na kisiasa. Dkt. Hans aliamini kwamba sababu za kiutamaduni zilichangia zaidi katika kuenea kwa UKIMWI. Aliamini kwamba ilikuwa vigumu kwa vijana waliofunzwa kikamilifu katika majando, kuingia kwenye uasherati kwa urahisi. Aliwachukulia vijana wa Kimaasai kama mfano mzuri, kwani kiwango cha ugonjwa huo kwa Wamaasai kilikuwa chini sana… (uk. 41).

Aidha, mwingiliano mkubwa wa watu unakisiwa kuwa mmojawapo wa mambo yaliyochochea kasi ya maambukizi haya. Mwandishi anarejelea hali ilivyokuwa jijini Dar es Salaam kwa kusema;

> Jiji la Dar es Salaam lilikuwa na mwingiliano mkubwa wa watu. Idadi kubwa ya vijana walikuwa wakihama kutoka vijijini kuja Dar es Salaam. Hii ilisababisha ongezeko kubwa la watu kuleta athari nyingine nyingi katika uhusiano baina ya watu, vipato vyao na utamaduni wa matumizi ya vipato hivyo. Jiji lilifura, likavuma na kustawi bila mpangilio. Hatua kwa hatua, ugonjwa wa UKIMWI uliunyemelea ustawi huo na kuanza kuula kutoka kwenye mizizi kuelekea kwenye shina na matawi yake. (uk. 42)

Tunaweza kusema kuwa kutokana na mabadiliko haya ya kiuchumi, watu waliotononoka kiuchumi walijichopeza katika anasa na starehe ilivyokuwa kwa Bwana Ngoma, Ito, Queen, Asha, Omolo na wengine. Waliokuwa wameoa kama Ngoma walijikuta katika mapenzi nje ya ndoa maarufu kama *mpango wa kando* nchini Kenya. Mahusiano haya nje ya ndoa na anasa ndiyo yaliyosababisha kusambaa kwa UKIMWI hata zaidi. Kwa mujibu wa Msimulizi, hali hii ilichangia katika kuzuka kwa mtandao wa maambukizi. Anaeleza haya kupitia mazungumzo baina ya wahusika Rajabu na Mpemba wakiwa katika hoteli ya Victoria:

> UKIMWI jama utatumaliza! Hebu fikiri idadi ya wanawake yule bwana alikuwa anazini nao!" Mpemba alimkatisha. "Aliokoteza mbegu kila mahali. Kwa Queen alichukua na kama huyu Asha kapewa mbegu na msafiri basi walipokutana na Ngoma walibadilishana mbegu…" Rajabu alieleza na kusisitiza kwa kupiga makofi. ( uk. 209).

**Maambukizi ya UKIMWI**

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na mpango wa taifa wa kudhibiti UKIMWI nchini Tanzania (TACAIDS, 2018-2019), maambukizi hutokea kwa njia kadhaa. Njia hizo ni pamoja na;

i. Kwa kujamiana na mtu aliyeambukizwa virusi vya UKIMWI. Njia hii ilichangia kwa 82.1% ya maambukizi;
ii. Kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (wakati wa ujauzito, wakati wa kujifungua au wakati wa kunyonyesha). Njia hii ilichangia 5.9% ya maambukizi.
iii. Kuongezwa damu yenye virusi vya UKIMWI. Njia hii ilichangia 3% ya maambukizi.
iv. Njia nyinginezo zilichangia 1.7% za maambukizi.
v. Kuambukizwa kutokana na chanzo kisichojulikana kulisababisha 10% ya maambukizi.

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* ambapo mwandishi ametumia mandhari ya Dar es Salaam, Tanzania, anaangazia zaidi suala la ngono bila kinga na mtu aliyeambukizwa virusi vya UKIMWI kama njia kuu ya kusababisha maambukizi haya. Takribani wahusika wote walioambukizwa ugonjwa huu wa UKIMWI kama Ngoma, Tabu, Queen, Msafiri na Asha waliambukizwa kupitia ngono bila kinga.

Yamkini ngono hii ya bila kinga ilisababishwa na ulevi pamoja na mapuuza ya wahusika wenyewe. Msimulizi anatueleza kuwa Queen na Asha walishiriki mahaba na Ngoma bila kujali matumizi ya kinga. Vilevile, wahusika kama Chiku na Pendo ambao wanakisiwa kuambukizwa ugonjwa huu, walishabikia mno ngono bila kinga na kupuuza matumizi ya mipira ya kinga (kondomu) katika tendo hilo. Hii inadhihirika wanapomzomea na kumfokea Jose, mhusika aliyekuwa na mazoea ya kunadi na kuuza kondomu katika baa ya Malaika. Kila mara Jose alipofika pale kuuza, alifukuzwa kwa matusi na masimango. Mwandishi anatueleza hivi;

> …Alipoingia Malaika akaanza kunadi biashara yake kwa kupaza sauti: …Mambo kwa soksi! Mambo kwa soksi!
>
> Maji uyavalie nguo ndipo uyakoge!
>
> Ulapo ndizi usiimenye ila ivishe ganda!
>
> Jando la raha leo ni kuvishana magozi!
>
> Aah! Hebu ondokee huku! Usitupigie kelele!" Chiku alimsogelea huku akimwonyesha njia atoke. Jose alimwepa, kisha akaenda katikati ya ukumbi. Akarudia maneno yake.
>
> Chiku na Pendo wakamshambulia kwa maneno, …wewe juzi ulipofungwa gerezani wenzio walipokuharibu walitumia mpira? (uk. 12)

Mtego huu wa maambukizi unanasa waliomo na wasiokuwemo. Tabu ambaye ni mtulivu katika ndoa yake, anaambukizwa ugonjwa huu na mumewe ambaye nyumbani hakumweki. Inaaminika kwamba Ngoma aliambukizwa virusi vya UKIMWI na Queen naye hatimaye akamwambukiza mkewe katika kitanda chao cha ndoa. Hatimaye Ngoma anajutia tendo tunavyofahamishwa katika mawazo yanayompitikia Ngoma akiwa na mkewe kitandani.

> …Ngoma pia hakuwa na tamaa tena ya kufanya mapenzi na mke wake, hasa alipojifikiria kwamba ana virusi vya UKIMWI na atakuwa anavipandikiza kwa mkewe. Lakini kilichomtia kinyaa zaidi na hasira za kujuta, ni lile wazo kwamba tayari ameshamwambukiza na hakuwa na jinsi yoyote ya kumwokoa kwa tiba (uk. 135).

Msimulizi anajaribu kueleza sababu hasa ya ngono bila kinga kuwa chanzo kikuu cha maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Kupitia kwa mhusika Jose, tunabaini kuwa sababu kuu ni kuwa watu wameingilia tabia ya kushabikia ngono na wala hawajali madhara yake. Jose anasema hivi;

> …Mimi naona ni busara zaidi kupiga vita vya watu kushabikia ngono kwenye sinema, kwenye miziki yote ya kiafrika, kila mahali ni hamasa ya ngono. Muziki umekosa maana zaidi ya kunengua na kuonyesha uhodari wa viuno vya ngono… (uk. 13).

Njia nyingine inayoelezwa kuwa inaweza kusababisha maambukizi ni mgusano wa jeraha la mtu aliyeambukizwa virusi vya UKIMWI na jeraha la mtu ambaye bado hajaambukizwa. Tunapata kujua hilo kutokana na kauli ya Dkt. Hans anapomshauri Shehe Rajabu kuhusu namna ya kumwosha maiti wa UKIMWI. Dkt. Hans anamweleza Shehe Rajabu kuwa;

> …Ni vizuri waoshaji wakivaa mipira ya kinga na kama kuna mwenye jeraha mikononi asioshe, kwa ajili ya usalama wake… (uk. 296).

**Athari za Maambukizi ya UKIMWI**

Kwa mujibu wa riwaya hii, athari ya maambukizi ya UKIMWI inadhihirika kupitia mabadiliko katika miili na hali ya kiafya ya waathiriwa. Mabadiliko haya yanawasababishia vifo baadhi ya wahusika kwa mfano Queen, Ngoma na Tabu. Vifo vyao vinasababisha jitimai na simanzi katika jamii zao. Vilevile, watoto wao wanakuwa mayatima.

UKIMWI unawaathiri na kuzorotesha hali yao ya kiafya. Queen, mwanamke mzuri, mrembo, mwanasheria mtajika na mwenye mafanikio makubwa katika maisha ndiye wa kwanza anayeanza kuugua. Mwanzoni mwa hadithi Queen anaanza kuonyesha dalili za ugonjwa, wapenzi wake wote akiwemo Ngoma wanaanza kuogopa. Baada ya miezi minne, anaugua sana, mwandishi anaieleza hali yake hivi;

> Queen alikuwa amedhoofu sana. Mashavu yalikuwa yamebonyea, kifua kimesinyaa na ngozi yake ilikuwa imepauka na kuwa kama mtu aliyekuwa kwenye mavumbi … Fizi zilikuwa nyekundu mno, zenye dalili ya vidonda. Lile tabasamu la uzuri alilokuwa nalo zamani sasa lilikuwa limegeuka kuwa la kutisha. (Mkufya, 2004:157-158) … unene wote uliompa umbile zuri ulikwishasinyaa, amekuwa mweusi… weusi usiovutia. Alikuwa kama nuru ya mwili wake imeingia giza na sehemu zake za siri zilitoa harufu kali kutokana na vidonda vilivyomshambulia nje na ndani (uk. 166).

Kutokana na hali hii, mhusika huyu anatamauka na hatimaye anazuumu kujiangamiza mwenyewe. Mwandishi anatupa tafakari ya Queen kabla ya kujiua:

> Kwani maisha ni nini hasa? Kuishi miaka mia na kuishi miaka hamsini kuna tofauti gani? Au mimi ninayekufa leo na yule atakayekufa miaka mitano ijayo au ishirini baadaye kuna tofauti gani?... mtu anapotaka kujiua watu wanamkataza. Akikamatwa anaadhibiwa kifungo gerezani! Si upuzi tu! Mimi sioni tofauti yoyote kati ya kuwepo na kutokuwa (uk. 158).

Baada ya miaka minne, Asha, naye anaugua sana. Asha alikuwa mke wa mzungu tajiri, na anaacha mali yake mikononi mwa watoto mayatima ambao wazazi wao wamekufa kwa UKIMWI. Anafanya hivyo ili kuiokoa roho yake mbele ya safari.

> Katika miaka ile, ilikuwa msimu wa wanaume kupenda wanawake wanene, wenye matako makubwa na kifua kilichojaa maziwa. Asha alikuwa na kila sifa ya umbile hilo (uk. 16). Omolo alishtuka sana kuona jinsi Asha alivyopwaya na kukonda. Hakuamini kuwa huyo alikuwa yule Asha aliyemzoea, mwenye matako manene, maziwa yaliyofura na mabega yaliyokuwa imara (uk. 314).

Mhusika mwingine anayeathiriwa na maambukizi ya UKIMWI kiasi cha kuliwawa kiafya ni bwana Ngoma. UKIMWI uliuponda na kuutafuna mwili wake kiasi cha kumgeuza gofu la mtu. Msimulizi anaieleza hivi hali ya Ngoma:

> …Mwili wake mkubwa aliouzoea toka zamani sasa ulikuwa umesinyaa na kuwa kama wa mtoto. Kichwa kilikuwa kimekonda na nywele zilinyonyoka na kuacha msitu wa ndevu zilizochanwa (uk. 280).

Vilevile, Ngoma anapomtazama mkewe, Tabu na kutathmini hali yake, anaona mabadiliko makubwa katika afya ya mkewe yaliyosababishwa na UKIMWI.

> Ngoma akamtazama mkewe, kumbukumbu za maisha ya huko nyuma toka walipooana zikamrudia. Hakika, ule ulikuwa wakati wa furaha na mapenzi. Tabu alikuwa mwanamke wa

> kuvutia aliyeweza kumshutua mwanamume yeyote jijini. Sasa wote wamechakaa, sura zao zimenyauka na miili yao imechoka (uk. 279).

Hatimaye katika hadithi hii, wazazi hawa wawili (Ngoma na Tabu) wanafariki dunia na kuwaacha watoto wao mayatima. Tunaelezwa pia katika hadithi kuwa kulikuwepo na watoto wengine mayatima ambao wazazi wao waliangamizwa na UKIMWI. Hali hii ndiyo inayompelekea Omolo, Asha na Catherine Hastings kuanzisha hazina au benki ndogo itakayosaidia watoto yatima ambao yamkini wazazi wao walikufa kwa UKIMWI (Mkufya, 2004:307).

Aidha, Chiku na Msafiri wanapougua UKIMWI afya yao inazorota na kuwalazimu kuacha kazi. Hatimaye wanarejea vijijini kujiuguza. Msimulizi anatudokezea hali yao baada ya kuambukizwa.

> Chiku akaanza kuugua magonjwa mbalimbali…kulikuwa na tetesi kwamba alikumbwa na UKIMWI … Chiku alirudishwa kwao Tabora akiwa amedhoofu sana (uk. 203).

Kumhusu Msafiri, tunaelezwa hali yake baada ya kuambukizwa UKIMWI. Akiwasiliana na Zito Mpemba anamweleza hivi:

> Naskia alianza kukohoa, akakonda sasa alipoanza kuharisha, waliomjua wakamtoa hospitalini na kumkodishia gari wakamrudisha kwao, Shinyanga (uk. 206).

**Njia za Kuepuka Maambukizi ya UKIMWI**

Kwa mujibu wa riwaya hii, msimulizi amependekea njia kadha wa kadha za kujikinga na UKIMWI. Njia ya kwanza inayopigiwa debe mwanzoni mwa hadithi kupitia kwa mhusika Jose, ni kupiga vita tabia za kushabikia ngono. Vilevile, iwapo udhibiti wa kushabikia ngono hauwezi kusibu, basi mwandishi anawashauri watu wanapofanya mapenzi au kitendo cha ngono siku zote wasikose kutumia mpira wa kinga au kondomu. Aidha, anawaonya pia watu wanaohusika na kuosha maiti wasisahau kuvaa glavu mikononi ili mfu wa UKIMWI asiwaambukize virusi iwapo wote wana majeraha.

Njia nyingine inayodhihirika katika mjadala baina ya Grace na Dkt. Hans ni kuoga kwa sabuni nyingi iwapo mpira umechanika wakati ambapo mtu anashiriki ngono na mwathiriwa wa UKIMWI. Dkt. Hans anamweleza Grace kwamba:

> …Utetezi kwamba alioga kwa sabuni nyingi ni kweli, kitaalamu wadudu wale huliwa na sabuni… (uk. 257)

Hata hivyo, mwandishi anahitimisha kwa kudai kuwa njia mwafaka ya mtu kujikinga dhidi ya UKIMWI ni kujua hali yake. Anaamini kuwa ni jambo bora mtu kujipima mwanzo ili ajijue. Kujijua kutamsaidia kuratibia mustakabali wa maisha yake vizuri na kuepuka kuwaambukiza au kuambukizwa na watu wengine.

**Matumaini kuhusu UKIMWI**

Maudhui yanayotamalaki katika hadithi hii ni masuala yanayoendana na UKIMWI. Hata hivyo, masimulizi yanayotolewa kuhusu ugonjwa huu yanaelezwa kwa njia ya kujenga matumaini makubwa miongoni mwa wahasiriwa. Mwandishi anaonyesha kwamba ugonjwa wa UKIMWI si hukumu ya maisha bali ni hatua ya kubadili mkondo wa maisha kwa waathiriwa. Anaeleza kuwa mwathiriwa wa UKIMWI akipata matibabu mazuri anaweza kuishi zaidi ya miaka kumi baada ya dalili za mwanzoni za maambukizi ya ugonjwa huu kujitokeza.

Vilevile, mwandishi anawashauri wale ambao bado hawajaambukizwa kuwa waangalifu wanaposhiriki ngono kwa kutumia kinga ili waepuke UKIMWI. Mwisho, mwandishi anatoa ujumbe wa matumaini hata kwa watu wanaokaribia kufa. Falsafa yake ni kwamba, wahasiriwa ambao wana watoto kizazi chao hakiwezi kupotea kabisa. Kwamba, maisha yao yataendelea hata baada ya kifo.

**Hitimisho**

Tunahitimisha makala haya kwa kurejelea kauli ya Bertoncini kumhusu mwandishi William Mkufya na mchango wake katika kuielimisha jamii. Bertoncini anasema hivi: *William Mkufya amerejea na*

*riwaya ya kiuhalisia, ambayo imechukua dhima ya mwalimu na kuelimisha jamii. Riwaya hii imejitwika dhima au jukumu kubwa la kuzungumzia suala nyeti la UKIMWI ambalo limekuwa kizungumkuti si tu katika bara la Afrika bali hata kwingineko. Katika kulizungumzia suala hili mwandishi amekuwa makini mno kuuelekeza umma kuyaepeka maambukizi na vilevile kutowabagua watu ambao tayari walikwishaathiriwa na UKIMWI (Bertoncini. 2005:3)".*

Katika makala haya ni wazi kuwa mwandishi wa *Ua la Faraja* ameonyesha kuwa UKIMWI ni ugonjwa tu wa kawaida kama magonjwa mengine kwa hivyo kuambukizwa UKIMWI si kutolewa hukumu ya kifo. Anawashauri watu kupimwa ili kujua hali zao kuhusu janga la UKIMWI, kufanya hivyo kutawawezesha kudhibiti makali ya maambukizi yake. Mwishoni mwa hadithi mwandishi anaonyesha kuwa kuna matumaini hata kwa waathiriwa wanaokaribia kufa kutokana na maambukizi ya UKIMWI. Kwa hivyo, kama tulivyotanguliza, riwaya hii ni zinduo, hamasisho na kichocheo si tu kwa taifa la Tanzania bali pia kote barani Afrika kuhusiana na juhudi zinazofaa kuchukuliwa katika kudhibiti maambukizi ya UKIMWI. Lau sivyo ugonjwa huu utadumaza maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika bara hili.

**Marejeleo**

Bertoncini, E. (2005) *William E. Mkufya's Latest Novel, Ua la Faraja: A commitment to the fight Against HIV/AIDS*.www.books, google.co.ke

https://www..tacaids,go,tz

https://www.who.int/news-room/q-a-detail/hiv-aids

Kandagor, M. (2012). Juhudi za Vyombo vya Habari Katika Kukuza na Kueneza Kiswahili Nchini Kenya-Jarida la Kioo cha Lugha-Dar-es-Salaam. Juz. 10. Kur. 32-47. ISSN: 2141-6222.

Kandagor, M. (2013a). Nafasi ya Lugha na Vyombo Vingine vya Mawasiliano Katika vita dhidi ya UKIMWI . *Jarida la Kioo.* Juzuu 11. Kur. 90-104. TATAKI: Dar-es-Salaam. ISSN: 0856-552X

Mkufya, W. E. (2004). *Ua la Faraja: Riwaya*. Dar es Salaam: Mangrove Publishers.

Ngugi, P.M. (2012). *Mitaala ya Kiswahili katika elimu na Utaifa: Nafasi ya Fasihi ya Watoto katika uendelezaji wa Utaifa.* (Wah.) Kimani Njogu, Clara Momanyi na Mwenda Mukuthuria. Uk 106-120. Nairobi: Twaweza Communication Ltd.

Njogu, K na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Openlibrary.org/.../Kamusi_ya_karne_ya_21

Simiyu, F. W. (2020). *Safina ya Utafiti wa Fasihi Simulizi.* Kakamega: Elgon Epitome Publishers Ltd.